# SIMU JANJA ZAONGEZEKA - FURSA UCHUMI WA KIDIJITI

*Na Mwandishi Wetu*

MATUMIZI ya simu janja yanaendelea kukua nchini, huku umiliki wa simu hizo ukionyesha ukuaji endelevu, kwa mujibu wa ripoti mpya ya robo mwaka ya kwanza ya takwimu za sekta ya Mawasiliano inayotolewa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). Ripoti hiyo inaonyesha kuwa matumizi ya simu za mkononi yameongezeka kutoka asilimia 92.7 mwezi Juni hadi asilimia 99.3 mwezi Septemba mwaka huu.



Akifafanua kuhusu takwimu hizo jijini Dar es Salaam hivi karibuni, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, alisema idadi ya watumiaji wa simu janja imeongezeka kutoka asilimia 36.75 mwezi Juni hadi asilimia 39.53 mwezi Septemba 2025.




**Dkt. Jabiri K. Bakari** | Mkurugenzi Mkuu - TCRA

Kufikia Septemba, jumla ya vifaa vinavyotumika kwa mawasiliano ya simu vilifikia milioni 58.85, ambapo milioni 26.94 kati ya hizo ni simu janja.

Dk. Bakari alibainisha kuwa ongezeko hilo la matumizi ya simu janja linafungua fursa mpya kwa watu binafsi na biashara, ikiwemo ufanyaji biashara mtandaoni, upatikanaji wa elimu ya kidijitali, na kuongeza tija katika uzalishaji.

"Watanzania wengi sasa wanatumia simu janja kuendesha biashara mtandaoni, kutangaza bidhaa zao na kujifunza vitu vipya," alisema Dk. Bakari.




Katika kuonyesha mafanikio hayo, watumiaji mbalimbali wameeleza kuridhishwa na maendeleo ya teknolojia ya mawasiliano nchini.

"Kupitia simu yangu, sasa naweza kuuza nguo kwa wateja walioko maeneo mbalimbali nchini," alisema Neema, mfanyabiashara kutoka Mwanza. "Hapo awali nilitegemea wateja waliokuja dukani pekee."

Nae Mwasampeta Aloyce mkazi wa Uyole Mbeya alifafanua umuhimu wa kuwa na simu janja kwa kizazi cha leo "Simu janja husaidia katika mawasiliano ya haraka, kupata intaneti, kujifunza, na kupata burudani. Pia hurahisisha biashara, malipo ya kifedha, na huduma za kibenki. Inasaidia kupata ramani na usafiri, kupiga picha, kufuatilia afya, na hata kutoa msaada wa kiusalama. Kwa ujumla, simu janja ni zana yenye nguvu ya kuunganisha ulimwengu, kuongeza ufanisi na kurahisiha maisha.

**Miundombinu ya Mawasiliano Yaendelea Kuongezeka**

Ripoti inaonyesha kuwa kufikia Septemba 2025, kulikuwa na minara ya mawasiliano 9,745 nchini, huku Dar es Salaam ikiongoza kwa kuwa na minara 1,225. Ongezeko hili limeboresha upatikanaji wa mtandao na ubora wa huduma za sauti na data katika mikoa mbalimbali.

"Tumeona ongezeko kubwa la upatikanaji wa intaneti, jambo ambalo limeongeza huduma Jumuishi kati ya mijini hadi vijijini, ambapo awali kulikuwa na ombwe la kidijitali baina ya wakazi wa mijini na vijijini," alisema Isaiah Mussa, mtaalamu wa TEHAMA.

Ripoti hiyo imebainisha pia ongezeko la watumiaji wa intaneti kwa asilimia 4.1, kutoka milioni 54.1 mwezi Juni hadi milioni 56.3 mwezi Septemba 2025. Huduma ya intaneti inapatikana kupitia data za simu, mkongo wa taifa, na mitandao isiyotumia waya (wireless). Idadi ya watumiaji imeongezeka kwa asilimia 5.5 tangu Desemba 2024.

"Katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, kila ongezeko la asilimia 10 la upenyaji wa intaneti linachangia hadi asilimia 2 ya ukuaji wa Pato la Taifa (GDP). Hii siyo tu kuhusu mtandao, bali ni kuhusu uwezeshaji wa kiuchumi," alieleza



Dr.Ndumbaro, Mchumi na mkazi wa Dar es Salaam.


**Ukuaji wa Teknolojia Mbalimbali**

Tanzania inaendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano kupitia teknolojia mbalimbali za kizazi cha 2G, 3G, 4G, na 5G. Ripoti inaonyesha kuwa: 2G inafikia asilimia 98.6 ya watu, 3G inafikia asilimia 93.8, 4G inafikia asilimia 94.2, na 5G sasa inafikia asilimia 28, kutoka asilimia 26 mwezi Juni 2025.

Dar es Salaam inaendelea kuwa kitovu cha mawasiliano nchini, ikiwa na idadi kubwa zaidi ya mitambo ya 2G, 3G, 4G na 5G.

"Mtandao wa kasi ya 5G umeleta mageuzi makubwa katika mawasiliano kwa kuwezesha mtandao wa kasi ya juu, usiokuwa na ucheleweshaji wa taarifa na uwezo wa kuunganisha vifaa vingi kwa wakati mmoja." Alisema Mhandisi Charles Thomas. Teknolojia hii imewezesha matumizi ya magari yanayojiendesha, huduma za afya kwa mbali (Telemedicine), miji ya kisasa (smart cities), na biashara mtandaoni. "Kwa ujumla, 5G inaongeza ufanisi, ubunifu, na maendeleo ya kiuchumi kwa kuboresha upatikanaji wa intaneti na huduma za kidijitali duniani". Aliongeza Mhandisi Charles Thomas


"Mtandao wa 5G ni wa kasi ya ajabu," alisema Moses Kasmiri, mtumiaji wa mtandao wa



intaneti jijini Dar es Salaam. "Kupakua mafaili makubwa kunachukua sekunde chache tu, jambo linalorahisisha kazi zangu za mtandaoni."

**Kuimarika kwa Huduma jumuishi za Kidijitali**

Ripoti inaonesha kumekuwa na ongezeko la umiliki wa simu janja na upatikanaji wa intaneti unaopelekea kuongezeka kwa huduma jumuishi za kidijitali, na kuwawezesha Watanzania wengi zaidi kushiriki katika uchumi wa kidijitali unaohusisha shughuli za elimu, afya, biashara, Ubunifu na mawasiliano kupitia mtandao.






Skani kupakua Ripoti ya Takwimu ya Sekta ya Mawasiliano